

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA SUMBAWANGA (SUMBAWANGA WSSA) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-027-2018/2019

Mnamo tarehe 21 Februari 2019 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Sumbawanga (Sumbawanga WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Majedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Unit)

Kundi la Wateja	Matu mizi (m ³)	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
		2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	0-5	800	139%	1,909	0.3%	1,914	0.4%	1921
	>5-<20	975	139%	2,326	0.3%	2,332	0.4%	2341
	>20	1,075	-	NA	-	NA	-	NA
Taasisi	0-5	1,000	77%	2,386	0.3%	2,392	0.4%	2,401
	>5-<20	1,155						
	>20	1,345						
Biashara	0-5	1,000	91%	2,386	0.3%	2,392	0.4%	2,401
	>5-<20	1,075						
	>20	1,250						
Viwanda	0-5	1,155	91%	2,756	0.3%	2,763	0.4%	2,773
	>5-<20	1,250						
	>20	1,440						
Magati	Lita 20	20	200%	60	0%	60	0%	60

Jedwali Na.2: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama Ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 24 ya Kanun za Maji za Mwaka 2013	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama Ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 24 ya Kanun za Maji za Mwaka 2013		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				

Jedwali Na.3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	15,000	33%	20,000	10%	22,000	14%	25,000
Taasisi	30,000	17%	35,000	6%	37,000	5%	39,000
Biashara	30,000	17%	35,000	6%	37,000	5%	39,000
Viwanda	30,000	17%	35,000	6%	37,000	5%	39,000

Jedwali Na 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuondoa Majitaka (TZS/Gari)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Majumbani	57,000	40%	80,000	0%	80,000	13%	90,000
Taasisi	69,000	30%	90,000	11%	100,000	20%	120,000
Biashara	69,000	30%	90,000	11%	100,000	20%	120,000
Viwanda	69,000	74%	120,000	25%	150,000	7%	160,000

Jedwali Na 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuwaga Majitaka katika Mabwawa ya Sumbawanga WSSA (TZS/Gari)

Aina ya Gari	Tozo ya Sasa	Tozo Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22
Tani 3 had 5	7,000	43%	10,000	50%	15,000	33%	20,000
Tani 7	10,000	50%	15,000	33%	20,000	25%	25,000
Tani 10	20,000	25%	25,000	20%	30,000	17%	35,000

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga sababu za kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni pamoja na uhitaji wa mapato ya kutosha kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo, kugharamia miradi ya uwekezaji na ununuzi wa vifaa, kuzipa pengo la mapato litokanalo na kuondolewa tozo ya huduma pamoja na kulipa tozo mbalimbali zilizopo kisheria.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 18 Aprili 2019** katika **Ukumbi wa Liboli**

Centre uliopo Sumbawanga Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Sumbawanga, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 19 Aprili 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI, GHOROFA YA SITA, JENGO LA NHIF; MTAA WA KARUME, MBEYA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SUMBAWANGA** zilizopo **SUMBAWANGA MJINI**.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)

29 Machi 2019